



Mic-Key® - Usafishaji na Utumiaji ukiwa nyumbani

Unashauriwa ufanye haya mara moja kwa siku:

1. Osha ngozi karibu na Stomi mara moja kwa siku, kama wakati unavyojiosha asubuhi au jioni. Ngozi karibu na Stomi inatakikana iwe imekauka na safi.
2. Osha vipande vya katikati na maji kiasi cha mililita 10-20 kabla na baada ya kulisha.

Unashauriwa ufanye haya mara moja kwa wiki:

1. Hakikisha kuwa kuna maji ya kutosha ndani ya mpira/baluni mara moja kwa wiki.
2. Badilisha vipande vya katikati mara moja (au mara nyingi kwa wiki; kutegemea na vile unavyovitumia)

Unashauriwa ufanye haya mara moja kila baada ya wikimbili:

1. Toa Mic-Key kutoka kwa stoma, ioshe kwa maji ya vuguvugu yaliyo na sabuni, kamua na ukaushe vizuri.

OBS! Inasaidia ukitumia Mic-Key®

Mbili, moja baada ya nyingine ili iwe rahisi kwako unapobadilisha, itakuwa haraka kusafisha na kubadilisha.

Unashauriwa ufanye haya mara moja kila baada ya miezi miliwi:

- Tumia Mic-Key® kama chombo cha kula chakula. Kwa hivyo badilisha Mic-Key® na kutumia mpya kila baada ya miezi miwili, kwa sababu itakuwa imebadilika rangi na chombo cha kuelekeza hewa safi kitakuwa kimeisha nguvu.

OBS, Ukisikia uchungu unapokula chakula, Wacha kula papo hapo na Ongea na daktari mara moja.





Ushauri Mzuri

1. Pima urefu sahihi wa stoma kwa kutumia Mic-Key® chombo cha kupimia. Kuwa na chombo cha kupimia kila wakati.
2. Tengeneza desturi au tabia ya kushafisha Mic-Key® saa fulani kwa mfano:
 - Hakikisha kuwa mpira au baluni ina maji ya kutosha kila jumatatu.
 - Toa Mic-Key® na kuishafisha kila jumatatu ya pili / kila baada ya siku kumi na nne.
3. Fikiria kuwa na usafi wa kawaida unapotumia chakula, usafishaji wa aina yote na kulisha Mic-Key®. Sio lazima ufuate taratibu ngumu za usafi zisizo za kawaida.